TAMKO LA JUKWAA LA ELIMU KWA MTOTO WA KIKE KUHUSU KAULI YA MH. HALIMA DENDEGO MKUU WA MKOA WA SINGIDA.

Utangulizi

Elimu ni haki ya kila mtoto nchini Tanzania, ni nguzo ya kupambana na umaskini, na ni nyenzo ya kuwawezesha watoto kufikia ndoto, kubadili fikra na kutatua changamoto zao na jamii. Serikali na wadau mbalimbali wameweka nguvu katika kuboresha mifumo ya elimu, ili kurahisisha upatikanaji wa elimu sawa kwa wote kama ilivyoanishwa kwenye **ibara ya 11** ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977.

Sisi, kama mashirika yanayounda jukwaa la elimu kwa mtoto wa kike, tumesikitishwa na kauli iliyotolewa na **Mh. Halima Dendego, Mkuu wa Mkoa wa Singida,** mnamo tarehe **21 mwezi Aprili 2024**, katika ziara yake ya kikazi katika Halmashauri ya wilaya ya Itigi alipokuwa akizungumza na wanafunzi wa shule ya sekondari Kitaraka. Tuna nukuu;

> "***Nikikuta msichana umepata mimba wewe utakuwa mshitakiwa namba Moja na wewe ndio utakayeenda jela bila huruma na tumbo lako utajifungulia huko huko kwa sababu mna tabia ya ukipata mimba tunaenda kukimbizana na mtoto wa kiume si sawa wote mlishirikiana kwa hiyo yeye atakuwa mshitakiwa namba mbili na msichana atakuwa mshitakiwa namba Moja".***

Aliendelea kwa kuagiza wanafunzi wa kike waliopata mimba wakiwa shuleni kukamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria pamoja na wazazi wao.

Kauli ya Mh. Dendego, inasahau chanzo cha mimba za utotoni katika jamii yetu na kuwahukumu wasichana kama ndio chanzo na suluhu pekee ya kumaliza tatizo la mimba za utotoni. Kauli hii inarudisha nyuma jitihada zinazochukuliwa na Serikali pamoja na wadau mbalimbali wa elimu katika kuhakikisha tunaondoa vikwazo na kila mtoto anapata fursa ya kupata haki ya elimu.

Sera na Sheria mbalimbali nchini

Sheria ya elimu katika kifungu cha 60 (3) (Sura ya 353 R.E 2019) kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2016 zinaeleza na kufafanua mazingira na adhabu atakayopewa mtu pale ambapo mwanafunzi amepata ujauzito Kifungu hicho kinasema

> "***Mtu yeyote ambaye amempa mimba mwanafunzi shule ya msingi au sekondari amefanya kosa na, atawajibika kwa kifungo cha kwenda jela muda wa miaka thelathini".***

Sheria ya Kanuni ya Adhabu sura ya 16 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2022 katika **kifungu chake cha 130 (1) (e)** kuwa mwanaume atakuwa amebaka pale atakapofanya tendo la ngono na binti wa umri chini ya miaka 18. Sheria hizi zote zinatoa ulinzi kamili kwa msichana wa miaka chini ya 18 na pia kwa mwanafunzi yeyote wa kike bila kujali umri, dhidi ya vitendo vya kingono, ili kumfanya afurahie haki

yake ya kielimu. Kumkamata binti aliyepata ujauzito ni kuendelea kumkandamiza yeye kama binti na pia yeye kama mhanga wa vitendo vya ubakaji alivyofanyiwa.

Mnamo, Novemba, 2021 Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST) ilitoa 'Waraka wa Elimu Na. 2, unaoruhusu wanafunzi waliokatiza masomo kwa sababu mbalimbali ikiwemo ujauzito kurejea shuleni katika mfumo rasmi. Serikali pia ilitoa mwongozo mnamo Februari, 2022 unaotaka wanafunzi kurejea shule ndani ya miaka miwili baada ya kuwa nje ya mfumo rasmi. Kwa mujibu wa takwimu za BEMIS 2022 na 2023 inaonesha wasichana 5,197 wameshareJea shuleni kama utekelezaji wa mwongozo huo. Hivyo, kwa uwepo wa mwongozo huu kuna maanisha serikali iko tayari kusaidia upatikanaji wa haki na usawa kwa watoto wote, ikiwemo wasichana waliokatiza masomo kutokana na mimba za utotoni

Maamuzi ya Kamati ya Wataalamu ya Haki na Ustawi wa mtoto katika shauri namba (ACERWC) 0012/Com/001/2019.

LHRC pamoja na CRR kwa niaba ya wasichana wa Tanzania walifungua shauri lilitolewa maamuzi na kamati kuhusu masuala mbalimbali ya uvunjifu wa haki za watoto ikiwemo suala la wasichana wa Tanzania waliokuwa wanakamatwa na kufungwa kwa kupata ujauzito kwani ni kuendelea kuwahukumu watoto ambao wamenyayaswa kingono, kubakwa na kufanyiwa Ukatili.

Kupitia shauri hilo Kamati ilitoa mapendekezo kwa Serikali ya Tanzania ikiwemo; pendekezo la kuhakikisha serikali inafanyia uchunguzi kesi za watoto wa kike waliowekwa gerezani kwa sababu ya mimba na kuhakikisha wanaaachiwa haraka na pia kuacha mara moja kuwaweka ndani na kuwakamata wasichana wanaopata ujauzito kwani ni uvunjifu mkubwa wa haki zao za msingi. Pia, Kamati ilipendekeza Serikali ya Tanzania kuwachukulia hatua watu wote wanaowabagua au kuwanyanyapaa wasichana kuhusu hali yao ya mimba, ndoa na masuala mengine.

Tanzania imepiga hatua kubwa katika suala hili na kwa muda mrefu tumeendelea kufurahia ulinzi wa wasichana wanaopata ujauzito na urejeshwaji wao mashuleni. Hata hivyo kauli hii ya Mkuu wa Mkoa wa Singida ina lengo la kurudisha nyuma harakati na juhudi za Serikali ya Tanzania, wadau wa maendeleo na watetezi wa haki za wasichana katika ulinzi wao kielimu. Suala hili pia linaenda kinyume na makubaliano ya utekelezaji wa mkataba wa Afrika wa haki na Ustawi wa mtoto ambao Tanzania imeridhia na hivyo kuirudisha Tanzania katika ramani ya wavunjifu wa haki za watoto Afrika.

HITIMISHO

Sisi kama jukwaa la elimu ya mtoto wa kike tunashauri mambo yafuatayo;

i. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST) kwa kushirkiana na wizara za kisekta kutoa ufafanuzi na maelekezo kwa watendaji kuhusu utoaji wa taarifa sahihi kuhusu utekelezaji na msimamo wa Serikali kikanda na kimataifa kwenye

suala la wasichana wenye ujauzito kurudi shule. Hii itasaidia baadhi ya viongozi kuacha kutoa kauli zinazoweza kuleta taharuki juu ya ulinzi wa haki za watoto.

ii. Tanzania kutekeleza mapendekezo ya shauri namba 012 la Kamati ya Wataalamu ya Haki na Ustawi wa Mtoto ili kutatua mizizi na chanzo cha wasichana kupata ujauzito na kumlinda ipasavyo mtoto wa kike.

iii. Tunatoa wito kwa viongozi na wadau kiujumla kuendelea kuelewa na kuheshimu sheria na miongozo juu ya ulinzi na usalama wa mtoto iliyowekwa na kujizuia kutamka misimamo binafsi kwani Tanzania inaongozwa na Katiba na sheria.

Imetolewa na Jukwaa la Elimu kwa Mtoto wa Kike.

Tarehe: 24/04/2024

Tanzania Education Network (TEN/MET)
Legal and Human Rights Centre
Children Dignity Forum (CDF)
Flaviana Matata Foundation
Child Support Tanzania
Msichana Initiative
Transforming Lives
Lyra in Africa
HakiElimu
WLAC
FAWE Tz
TGNP Mtandao